Msururu wa Upotofu na Udanganyifu

Kuweka wazi yanayotatiza

Toleo la (5)

Haiingii akilini!!



# MIMI NI MKAIDI?

SANAD

SW

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah. Rehema na Amani zimshukie Mtukufu wa manabii na Mitume, Bwana wetu Muhammad aliyetumilizwa ni rehema kwa viumbe, ziwashukie na jamaa zake na maswahaba zake wote.

Amesema Allah aliyetukuka:

{Pale walio kufuru walipo tia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga, Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya Waumini, na akawalazimisha neno la kuchamngu. Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu}[1].

{Nami sijitoi lawamani. Kwa hakika nafsi ni mno kuamrisha maovu, isipo kuwa ile ambayo Mola wangu Mlezi aliyo irehemu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Msamehevu na Mwenye kurehemu}[2].

Imepokewa kutoka kwa Jubayr bin Mut'im, Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: Si katika sisi atakaelingania kwa ukabila, si katika sisi atakaepigana kwa ajili ya ukabila, si katika sisi atakaekufa kwa ajili ya ukabila[3].



Ukaidi ni:


Kutokubali haki hata baada kudhihiri hoja kwa sababu ya kufuata mapendeleo ya kibinafsi.

(1) Al-Fath:26
(2)Yusuf:53
(3)Sunan Abi Dawud fi al-Adab

# Sifa za Mtu Mkaidi

Kwa maoni yako, ni nani mtu mkaidi? Na je tunaweza kujifanyia mtihani kwa haraka ili tuvumbue uwepo wa sifa hizi kwa kila mmoja katika sisi?

Chagua jibu lako baada ya kila sentesi, kisha ufuate maelekezo hapo mwisho. Jitahini na ujipime kuhusiana na sifa hii kupitia nukta hizi:



**Nakubali kutofautiana kimaoni wakati ninapojadiliana.**

**Maoni yangu ni sawa na haki, maoni ya mwengine ni makosa na batili.**

**Ninakosoa na kujadili fikra bila kumuingilia na kumkosea mwenye fikra.**

**Ninatafuta usawa bila ya kujifunga, na bila ya kuwa nimekinai na fikra fulani kabla.**

**Ninajadiliana na mwengine kwa mfumo wa kielimu na nakubali matokeo.**


**Nakubali sifa njema na misingi mizuri na nazinusuru hata kama zitatoka kwa anaetofautiana na mimi.**

**Namtambua mwengine awe atakavyokuwa na wala simdharau.**

**Kusifika kwa hizi sifa si jambo la rahisi, lakini ni kupanda daraja katika tabia njema, yastahiki tufanye juhudi dhidi ya nafsi zetu ili tufike.**

## Aina za Ukaidi

Ukaidi ni aina nyingi, na zinaweza kufungamana.




Mtume (rehema na amani zimshukie) alimsikia mmoja katika maswahaba kutokana na maanswari akilingania, “Enyi Maanswari!” na mmoja katika muhajirina akajibu, “Enyi muhajirina!” Mtume (rehema na amani zimshukie) akasema, “Kunani na ulinganizi wa kijahiliya?” Wakamwambia kuna mtu katika muhajirina amempiga mtu kutokana na maanswari, akasema:

**“Wacheni hilo kwani kwa hakika ni uvundo.”[4].**

4. Imepokewa na Bukhari na Muslim.

# Je unajuwa ya kuwa...




baadhi ya vita sababu yake ni ukaidi wa kivipote?



vita vya kilimwengu vya kwanza na vya pili ni kutokana na ukaidi wa kiuwananchi?



katika hatari kubwa zaidi ya athari za ukaidi wa kidini ni kupotoka na kutupa mipaka na kuenea fikra za kukufurisha katika jamii?




kifo cha baadhi ya washangiliaji michezo ilikuwa kwa ajili ya ukaidi wa soka?




## Natija za Ukaidi

Tukikosa kusameheana na ukaidi ukizidi, kulingana na maoni yako, je unaitakidi kuwa haya yanayofuata kwenye jedwali hapo chini yanaweza kupatikana?



- Kukiwepo fikra tofauti tofauti tutaweza kufikia uhakika wa mambo na hukumu ya sawa.
- Mtu akiwa amekinai na fikra fulani kabla kujadiliana, anapojadiliana huwa anafikia hukumu ya sawa na kwa haraka.
- Yataenea mapenzi na mazowea na kutaondoka utesi katika jamii pamoja kumkubali anaetofautiana na sisi.
- Jamii zitaimarika kielimu na kifikra na kijamii kwa ajili ya kuwa umoja wa maoni.
- Uislamu una uhuru wa kuchagua na haukubali kulazimishana katika dini na kubadilisha itikadi kwa hali yoyote, Hapana kulazimisha katika Dini.

### Kwani huitakidi kuwa...



kukubali tofauti ni dalili ya mwanadamu kupanda daraja

kuwepo maoni tofauti tofauti ni sababu ya maendeleo na kukuwa kwa jamii

kukosoa kwa ajili ya lengo zuri ni tabia nzuri ya hali ya juu

kuwepo na maoni mengi na kuyakubali ni dalili ya jamii iliyoendelea

## Ufupi wa Maneno

Kabla ya kusoma misimamo ya kielimu yalioafikanwa na yaliotafautianwa, tuna haja sana ya kusoma adabu za kupekua na tabia za kuzungumziana ili kupatikane kujadiliana kwa vizuri na kukinaishana badali ya vita na utesi. Na huo ndio mfumo wa Qurani ambao tunafaa kuufuata. Nao ni:

- Tujilazimishe kuwa na upole na adabu ya hali ya juu ili tuwe tunataka kufahamisha sio kushinda. Angalia uzuri wa kusema katika neno lake Allah: {Sema: Nyinyi hamtaulizwa kwa makosa tuliyoyafanya, wala sisi hatutaulizwa kwa mnayo yatenda nyinyi.}[5] Hakusema "kwa makosa munayoyafanya" kwa mkabala wa {makosa tuliyoyafanya}. Angalia wao wamejinasibishia makosa lakini wenzao hawakuwanasibishia makosa. Na huu ni upole wa aina ya juu sana katika kujadiliana.

- Tuanze maneno yetu pamoja na tunaepingana nae kwa msingi wa kukubali uwezekano wa kupatikana usawa ukitoka kwake hata kama ilikuwa tukiitakidi ni batili, na uwezekano wa kupatikana kukosa kutoka kwetu hata kama ilikuwa tukiitakidi ni sawa. Na yenye kuhukumu ni hoja na dalili na sio ukaidi na mapendeleo. Na nembo yetu pamoja na anaetofautiana nasi iwe {Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu ulio wazi.}[6]



(1) Saba`:25
(2) Saba`:24

# Msururu wa Upotofu na Udanganyifu

Mjumbe wa Allah (rehema na amani zimshukie na jamaa zake) amesema, "Wataipokea hii elimu [Dini] waadilifu katika kila watakaokuja. Wataiondolea upotofu wa waliopotoka na uvamivizi wa wabatilishaji na upotoshaji wa wajinga." (7).

Baadhi ya wenye fikra za makosa wamefahamu maneno ya Allah Mtakatifu na maneno ya Mtumi wake  kwa namna isiyoafikiana na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa wema waliotangulia wala haziendani na makusudio na misingi mikubwa mema ya Ujumbe wa Mungu.

Wakakusudia baadhi ya aya za Qur`ani Tukufu ambazo zilioteremka kwa ajili ya wasiokuwa waislamu wakazitumia kwa waislamu. Na wakatumia aya zilizokuja katika hali fulani wakazifanya ni za kutumiwa kila mahali. Na wakaharibu maana ya maneno ya Mungu na hadithi ya Mtume wake mtukufu kwa namna imepeleka kukita au kujengeka fahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kupatikane vitendo ambayo havina mafungamano na uislamu Dini ya Amani ya Kiislamu.

Tutajua kupitia msururu huu kuhusu upotoshaji uliopatikana katika maana za maneno ya Mungu na maneno ya Mtume wake waliouangukia wenye fikra hizi za makosa, na upotevu katika hukumu fulani, na kubeba fahamu za makosa ambazo zimewafanya wapambunakane na makusudio ya Mungu na Mtume wake na fahamu ya wema waliotangulia.

7-Hadithi mashhuri imesahihishwa na ibn Abdul Barr, na imepokewa kuwa Ahmad bin Hanbal amesema, "Ni hadithi sahihi."

دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION

سند
SANAD

www.sanad.network
facebook.com/sanadnetwork
twitter: @sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork